

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA NNE

06 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA NNE – TAREHE 06 APRILI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):

**21. MHESHIMIWA ABUBAKARI DAMIAN
ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvutia uwekezaji wa kilimo cha Uyoga kwa kutumia pumba za mpunga hasa katika Jimbo la Kilombero.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

22. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka Watumishi na vifaa muhimu kwenye Hospitali inayojengwa katika Mji wa Tunduma ili ianze kufanya kazi mapema;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Madaktari na Wakunga pamoja na kuongeza bajeti katika Kituo cha Afya cha Tunduma ili kukidhi mahitaji ya Kituo.

23. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Mradi wa kimkakati wa machinjio Iringa Ngelewala ili uwekezaji huo uanze kuleta tija kwa Taifa.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

24. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi ya muda mrefu ya ujenzi wa barabara kutoka Kilindi kwenda Gairo kwa kiwango cha lami.

25. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Kolandoto hadi Kishapu kwa kiwango cha lami utaanza.

WIZARA YA KILIMO:

26. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wakulima wa Jimbo la Singida Magharibi wanaoteswa na ndege aina ya Selengwa kula mazao yao na kuwarudisha nyuma kiuchumi.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

27. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzalisha mbegu bora za Kuku wa Kienyeji na kuhakikisha zinawafikia Wafugaji wa Kuku katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa bei nafuu ya ruzuku na kwa wakati.

28. MHESHIMIWA YAHAYA OMARI MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Malambo katika Halmashauri ya Itigi kwa ajili ya Wafugaji kunyweshea maji mifugo yao.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

29. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-


Je, Serikali inachukua hatua gani ya dharura kukabiliana na mrundikano mkubwa wa mahabusu katika Magereza nchini.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

30. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni vigezo gani hutumika kushindanisha ufaulu kwa Shule za Msingi na Sekondari kwa Halmashauri na Mikoa hapa nchini.



WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

31. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Uyui.

**DODOMA
06 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**